JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

______

# SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA
# SURA YA 83
# (TOLEO LA MWAKA, 2012)

## TOLEO LILILOREKEBIWA
## LA MWAKA, 2012

Toleo hili la Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sheria Namba 8 ya mwaka 2011 limezingatia na kuweka pamoja mabadiliko yote yaliyofanywa katika Sheria hii tangu ilipotungwa mwaka 2011 hadi tarehe 28 Februari, 2012 na limechapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Urekebu Sheria Sura ya 4.

Dar es Salaam,
28 Februari, 2012

**FREDERICK M. WEREMA**
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

# SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA
# (SURA YA 83 TOLEO LA 2012)

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Maelezo*


### SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina la Sheria.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

### SEHEMU YA PILI
MADHUMUNI

4. Madhumuni.

### SEHEMU YA TATU
UUNDAJI WA TUME

5. Uundaji wa Tume.
6. Uteuzi wa wajumbe wa Tume.
7. Muundo wa Tume.
8. Hadidu za Rejea.
9. Kazi za Tume.
10. Uhuru wa Tume.
11. Kiapo cha wajumbe na Katibu wa Tume.


.

12. Ukomo wa ujumbe.
13. Sekretarieti.
14. Gharama za Tume.
15. Kinga kwa wajumbe wa Tume na Sekretarieti.
16. Ukaguzi wa Hesabu zaTume.

## SEHEMU YA NNE
### UTARATIBU WA UTENDAJI KAZI WA TUME

17. Utaratibu wa utendaji kazi.
18. Mabaraza ya Katiba.
19. Ripoti ya Tume.
20. Uwasilishaji na uchapishaji wa ripoti.
21. Makosa na adhabu.

## SEHEMU YA TANO
### KUITISHA BUNGE MAALUM

22. Kuitisha Bunge Maalum.
23. Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.
24. Katibu na watumishi wa Bunge Maalum.
25. Mamlaka ya Bunge Maalum.
26. Masharti kuhusu Bunge Maalum.
27. Sheria za Bunge Maalum.
28. Ukomo wa mamlaka ya Bunge Maalum.
29. Gharama za Bunge Maalum.
30. Ukaguzi wa Hesabu za Bunge Maalum.

## SEHEMU YA SITA

### UHALALISHAJI WA KATIBA INAYOPENDEKEZWA

31. Uendeshaji wa kura ya maoni.
32. Swali la kura ya maoni.

33. Taarifa ya uendeshaji wa kura ya maoni.
34. Haki ya kupiga kura katika kura ya maoni.
35. Utaratibu wa kuendesha kura ya maoni.
36. Matokeo ya kura ya maoni.
37. Kuvunjwa kwa Tume.
38. Kuanza kutumika kwa Katiba.

MAJEDWALI

# SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA
# (SURA YA 83 TOLEO LA 2012)

[1st Desemba, 2011]
[ s.1(1)]

**Sheria kwa ajili ya kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba; kuainisha na kuchambua maoni ya wananchi; kuainisha masharti kuhusu mabaraza kutoa ushauri juu ya Rasimu ya Katiba; kuweka masharti juu ya utayarishaji na uwasilishaji wa ripoti kuhusu maoni ya wananchi; kuweka utaratibu wa kuunda Bunge Maalum, uendeshaji wa kura ya maoni na kuweka masharti yanayohusiana na mambo hayo.**

Sheria: Na.8 ya mwaka 2011
Na.2 ya mwaka 2012
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina la Sheria

**1**.-(1) Sheria hii itaitwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

(2) [Imeondolewa].

Matumizi

**2**. Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

Tangazo la Serikali Na. 394 la mwaka, 2011 Amri ya 2 aya (b), (c) na (d)

"Bunge Maalum" maana yake ni Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoundwa chini ya kifungu cha 22;

"katiba" maana yake ni sheria ya msingi, iliyoandikwa au isiyoandikwa, ambayo inaweka mfumo wa taifa kwa kuainisha misingi ya taifa ambayo jamii italazimika kuifuata, mgawanyo wa madaraka na majukumu ya mihimili mikuu ya dola, kwa kuainisha muundo wa serikali, bunge na mahakama, usimamizi wake mgawanyo na ukomo wa mamlaka ya vyombo mbalimbali vya dola, na kwa kuainisha namna na taratibu za utekelezaji wa mamlaka ya vyombo hivyo;

Sura ya 2

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977;

"Katiba inayopendekezwa" maana yake ni Rasimu ya Katiba iliyopitishwa na Bunge la Katiba kwa ajili ya kupigiwa kura ya maoni;

"Katibu" maana yake ni Katibu aliyetajwa chini ya kifungu cha 13;

"kura ya maoni" maana yake ni kura iliyopigwa na wananchi kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii kwa madhumuni ya kuridhia Katiba inayopendekezwa;

"mapitio ya katiba" maana yake ni mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kwa madhumuni ya kutunga upya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"mabaraza" maana yake ni mikutano, mikusanyiko, hadhara au majadiliano huru na ya wazi yaliyotayarishwa au kuandaliwa na Tume kwa madhumuni ya kutoa ushauri juu ya Rasimu ya Katiba;

"maoni ya wananchi" maana yake ni mawazo, maoni, fikira, taarifa au mapendekezo yaliyokusanywa kutoka kwa wananchi kwa madhumuni ya mchakato wa mabadiliko ya katiba;

Sura ya 2

"Rais" maana yake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"Tume" maana yake ni Tume iliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi kuhusu mchakato wa mabadiliko ya katiba;

"Waziri" maana yake ni Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano mwenye dhamana ya mambo ya katiba.

## SEHEMU YA PILI
### MADHUMUNI

Madhumuni

Tangazo la Serikali Na. 394 la mwaka, 2011 Amri ya 2 aya (e)

**4.-**(1) Madhumuni ya Sheria hii yatakuwa ni:

(a) kuweka utaratibu wa kuunda Tume itakayoratibu na kukusanya maoni ya wananchi;

(b) kuainisha viapo au yamini na kuweka taratibu kuhusu namna wajumbe wa Tume na Sekretarieti watakavyoapa au kula yamini;

(c) kuweka masharti kuhusu Hadidu za Rejea za Tume;

(d) kuweka masharti ya kuundwa kwa Sekretarieti ya Tume itakayoongozwa na Katibu;

(e) kuweka utaratibu ambao utaruhusu wananchi kushiriki kwa uwazi na kwa mapana katika kutoa na kuwasilisha maoni yao kuhusu katiba;

(f) kuweka utaratibu ambao Tume itautumia katika kutayarisha na kuwasilisha ripoti;

(g) kuainisha majukumu na mamlaka ya Tume;

(h) kuweka utaratibu kuhusu namna ambavyo Tume itakusanya maoni kutoka katika taasisi za umma na binafsi, vyama vya hiari na mashirika ya kidini, vyama vya siasa na makundi mengine kama ambavyo Tume itaona inafaa;

(i) kuweka utaratibu utakaowezesha Tume kupata taarifa za kitaalam kutoka kwa wataalam elekezi;

(j) kuweka utaratibu utakaowezesha kujenga muafaka wa kitaifa katika masuala yenye maslahi kwa taifa wakati wa mchakato kuhusu katiba;

(k) kuweka utaratibu utakaowezesha kuchambua Rasimu ya Katiba;

(l) kuweka mfumo wa kisheria utakaomwezesha Rais kuitisha Bunge Maalum;

(m) kuweka mfumo utakaowezesha uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum na upatikanaji wa Katibu na watendaji wengine;

(n) kuweka mfumo wa kisheria utakaowezesha kupiga kura ya maoni; na

(o) kuweka utaratibu wa namna ambavyo Katiba Mpya itakavyozinduliwa.

(2) Mchakato wa kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi, majadiliano katika mabaraza na katika Bunge Maalum na ushiriki katika kura ya maoni itawahusu wananchi ambao ni raia wa Tanzania pekee.

## SEHEMU YA TATU
### UUNDAJI WA TUME

Uundaji wa Tume
Amri ya 2 aya (f)

**5**. Rais, baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar, na kwa kuzingatia hali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi iliyopo katika Jamhuri ya Muungano, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, ataunda Tume.

Uteuzi wa wajumbe wa Tume

**6**.-(1) Rais, baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar, atateua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume.

Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3), muundo wa Tume utazingatia msingi wa kuwepo kwa uwakilishi ulio sawa kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.

Amri ya 2 aya (g)

(3) Katika kufanya uteuzi wa wajumbe wa Tume, Rais atazingatia masuala yafuatayo:

Sheria Na.2 ya Mwaka 2012 kif.2

(a) uzoefu katika kufanya mapitio ya katiba na sifa za kitaaluma za wajumbe kwenye mambo ya katiba, sheria, utawala, uchumi, fedha na sayansi ya jamii;
(b) jiografia na mtawanyiko wa watu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na
(c) umri, jinsia na uwakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii.

(4) Bila ya kuathiri ibara ndogo ya (3), mtu hatakuwa na sifa ya kuteuliwa kama mjumbe wa Tume isipokuwa kama ni mwaminifu wa hali ya juu na ana tabia isiyotiliwa shaka na jamii.

(5) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (3), mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume endapo mtu huyo:

(a) ni mtumishi katika vyombo vya usalama;

(b) ni mtu aliyewahi kuhukumiwa kwa kutenda kosa, au ni mtuhumiwa katika shauri lililopo mahakamani linalohusu shitaka la kukosa uaminifu au maadili; au

(c) si raia wa Tanzania.

(6) Kwa madhumuni ya vifungu vidogo vya (1), (2) na (3), Rais ataalika vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu, jumuiya za kidini, asasi za kiraia, jumuiya, taasisi zisizo za kiserikali na makundi ya watu wenye malengo yanayofanana kuwasilisha orodha ya majina ya watu ili kuteuliwa kuwa wajumbe.

Isipokuwa orodha hiyo itapaswa kuonyesha, kwa kila jina linalopendekezwa, umri, jinsia, uzoefu, sifa na mahali anapotoka mtu huyo.

(7) Kifungu kidogo cha (6) hakitatafsiriwa kuwa kinamzuia Rais kuteua kuwa wajumbe watu wasiokuwemo kwenye orodha ya majina yaliyowasilishwa kwake kama inavyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (6).

Muundo wa Tume
Tangazo la Serikali Na.394 la Mwaka 2011 Amri ya 2 aya (h)

**7**.-(1) Tume itakuwa na Wajumbe kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti;

(b) Makamu Mwenyekiti; na

(c) Wajumbe wengine wasiozidi thelathini na wasiopungua ishirini.

(2) Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti utafanyika kwa msingi kwamba iwapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atakuwa ni mtu anayetoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Wajumbe wa Tume watateuliwa kupitia amri itakayotangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Hadidu za Rejea

Tangazo la Serikali Na. 394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (i)

**8**.-(1) Hadidu za rejea za Tume zitakuwa kama zilivyoainishwa katika vifungu vya 9 na 17 vya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kushughulikia jambo lolote kama itakavyoona inafaa katika kutekeleza majukumu yake.

(3) Tume itakamilisha kazi yake ndani ya kipindi kisichozidi miezi kumi na nane kuanzia tarehe ya kuanza kazi.

(4) Endapo Tume itashindwa kukamilisha kazi yake ndani ya kipindi kilichoelezwa katika kifungu kidogo cha (3), Rais, kwa
makubaliano na Rais wa Zanzibar, anaweza kuongeza muda usiozidi miezi miwili ili kuiwezesha Tume kukamilisha na kuwasilisha ripoti.

Kazi za Tume

Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (j)

**9**.-(1) Majukumu ya Tume yatakuwa ni-

(a) kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi;
(b) kupitia na kutafiti usahihi na ulinganifu wa masharti ya kikatiba yanayohusu mamlaka ya wananchi, mifumo ya kisiasa, demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora;
(c) kutoa mapendekezo kwa kila hadidu ya rejea; na
(d) kuandaa na kuwasilisha ripoti.

(2) Katika kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume itaongozwa na misingi mikuu ya kitaifa na maadili ya jamii ya kuhifadhi na kudumisha mambo yafuatayo:

(a) kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano;
(b) uwepo wa Serikali, Bunge na Mahakama;
(c) mfumo wa kiutawala wa kijamhuri;
(d) uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
(e) umoja wa kitaifa, amani na utulivu;

(f) uchaguzi wa kidemokrasia wa mara kwa mara katika vipindi maalum kwa kuzingatia haki ya watu wote wenye sifa ya kupiga kura;
(g) ukuzaji na uhifadhi wa haki za binadamu;
(h) utu, usawa mbele ya Sheria na mwenendo wa sheria; na
(i) uwepo wa Jamhuri ya Muungano isiyofungamana na dini yoyote na inayoheshimu uhuru wa kuabudu.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2), na kwa jambo lolote jingine muhimu kwa Taifa, Tume itatoa fursa kwa wananchi kutoa maoni yao kwa uhuru kwa lengo la kuendelea kuboresha masuala hayo.

Uhuru wa Tume

**10**. Tume itakuwa na mamlaka na uhuru kwa kadri itakavyokuwa muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na mamlaka yake chini ya Sheria hii na haitaingiliwa na mtu au mamlaka yoyote.

Kiapo cha wajumbe na Katibu

**11**. Kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake, kila mjumbe wa Tume na Katibu ataapa au kula yamini mbele ya Rais kwa namna ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii.

Ukomo wa ujumbe

Sheria Na.2 ya mwaka 2012 kif.3

**12**.-(1) Mtu atakoma kuwa mjumbe wa Tume endapo litatokea tukio lolote kati ya matukio yafuatayo:
(a) kifo;
(b) kujiuzulu;
(c) kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu za kiafya;
(d) kuondolewa kwa makosa ya kukiuka Kanuni za Maadili;

(e) kutiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifungo gerezani kwa muda usiopungua mwezi mmoja; au

(f) kupoteza sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume, kutakuwa na kanuni za maadili kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria hii.

(3) Mjumbe wa Tume ambaye atakiuka masharti ya Kanuni za Maadili atapoteza sifa za kuendelea kuwa mjumbe.

(4) Endapo suala la kumuondoa mjumbe kwa kukiuka Kanuni za Maadili litajitokeza, Rais atateua Kamati itakayoundwa na:

(a) Jaji wa Mahakama ya Rufani ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(c) Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(d) Wakili wa Mahakama Kuu Zanzibar atakayependekezwa na Chama cha Wanasheria Zanzibar; na

(e) Wakili wa Mahakama Kuu atakayependekezwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika,

na Kamati hiyo itafanya uchunguzi wa suala hilo na kisha kutoa mapendekezo yake kwa Rais, na endapo Kamati itapendekeza kuwa mjumbe huyo asiondolewe, suala la kumuondoa mjumbe huyo litasita.

(5) Kamati itatengeneza utaratibu wa kufanya uchunguzi.

Sekretarieti

**13**.-(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Tume itakayoongozwa na Katibu akisaidiwa na Naibu Katibu.

Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (k)

(2) Katibu na Naibu Katibu watateuliwa na Rais baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar kwa msingi kwamba, iwapo Katibu anatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Naibu Katibu atakuwa mtu anayetoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.

Sheria Na.2 ya mwaka 2012 kif.3

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu au Naibu Katibu endapo mtu huyo ni mtumishi wa Serikali na ana taaluma ya sheria na amefanya kazi hiyo kwa muda usiopungua miaka kumi na ana mwenendo na tabia nzuri.

(4) Katibu na Naibu Katibu watawajibika kwa Tume na watafanya kazi na kutekeleza majukumu ya Sekretarieti.

(5) Watendaji wengine wa Sekretarieti watateuliwa na Waziri kwa makubaliano na Waziri mwenye dhamana ya mambo ya Katiba wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(6) Sekretarieti itakuwa na idadi ya watumishi wa umma kwa kadri itakavyohitajika kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu na matumizi ya mamlaka ya Tume.

(7) Tume itakuwa mamlaka ya nidhamu kwa wajumbe wa Sekretarieti.

Gharama za Tume

**14**.-(1) Gharama za shughuli za Tume wakati wa mchakato wa mapitio ya katiba kwa mujibu wa Sheria hii zitalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Wajumbe wa Tume na Sekretarieti watalipwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi.

Kinga kwa wajumbe wa Tume na Sekretarieti

**15**. Mjumbe wa Tume au Sekretarieti hatashitakiwa yeye binafsi kwa shauri la madai au jinai kutokana na jambo lolote au kitu chochote atakachofanya au kutofanya kwa nia njema kama mjumbe wa Tume au Sekretarieti katika utekelezaji wa majukumu na utumiaji wa mamlaka yake chini ya Sheria hii.

Ukaguzi wa Hesabu za Tume
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011

**16.**-(1) Katibu atahakikisha kwamba vitabu vya hesabu vinahifadhiwa na kwamba, ndani ya muda usiozidi miezi mitatu baada ya kwisha mwaka wa fedha wa Serikali, taarifa ya mapato na matumizi katika mwaka wa fedha husika inaandaliwa.

Sura ya 418, 410 na 348
Amri ya 2 aya (l)

(2) Hesabu zinazohusu kazi za Tume hadi siku ya mwisho ya mwaka wa fedha wa Serikali zitawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sheria ya Ununuzi wa Umma na Sheria ya Fedha za Umma.

## SEHEMU YA NNE
### UTARATIBU WA UTENDAJI KAZI WA TUME

Utaratibu wa utendaji kazi
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011
Amri ya 2 aya (m)
Sheria Na.2 ya mwaka 2012 kif.3

**17.**-(1) Tume itatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii na hadidu za rejea.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu kidogo cha (1), Tume itafanya kazi zifuatazo:

(a) kuandaa na kuendesha programu za kuelimisha juu ya madhumuni na majukumu ya Tume;

(b) kuitisha na kusimamia mikutano au mabaraza katika sehemu na nyakati mbalimbali kama itakavyoamua;

(c) kutathmini na kuchambua kwa kutofautisha maoni ya wananchi yanayokubaliana na yale yasiyokubaliana; na

(d) kutayarisha na kuwasilisha ripoti kwa kuzingatia hadidu za rejea.

(3) Tume yaweza kumtaka mtu yeyote atakaye hiari kufanya hivyo kwenda mbele ya Tume kufanya majadiliano, kwa mazungumzo au kuwasilisha nyaraka, kuhusu jambo lolote la kikatiba ambalo Tume inaona ni muhimu na linahusiana na mchakato wa mabadiliko ya katiba.

(4) Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, Tume itapitia na kuchambua michango, mawazo, maoni, taarifa na mapendekezo yaliyokusanywa na kufanyiwa tathmini siku za nyuma ikiwemo:

(a) muhtasari wa maoni ya wananchi kwenye maeneo wanayokubaliana na wasiyokubaliana kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano;

(b) nyaraka zote zinazowakilisha mawazo, maoni ya wananchi kwa ujumla katika Waraka wa Serikali Na.1 wa mwaka 1962 kuhusu kuanzishwa kwa Jamhuri ya Tanganyika, Azimio la Arusha la Mwaka 1967, Tume ya Rais Kuhusu Kuanzishwa kwa Mfumo wa Kidemokrasia wa Chama Kimoja, Mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya CCM ya mwaka 1983 kuhusu Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979, Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Tanzania ya mwaka 1991 na Kamati ya Kukusanya Maoni Kuhusu Katiba (Waraka wa Serikali Na.1 wa mwaka 1998);

(c) Katiba ya Uhuru wa Tanganyika ya mwaka 1961;

(d) Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya mwaka 1962;

(e) Hati za Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar;

(f) Katiba ya Mpito ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1965;

Sura ya 2

(g) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya

mwaka 1977;

(h) Presidential Decrees of Zanzibar zifuatazo:

(i) The Constitutional Government and the Rule of Law Decree,1967;

(ii) Equality, Reconciliation and Unity of the Zanzibar People Decree, 1964;

(iii)

(iv) The Existing Laws Decree, 1965;

(v) Confiscation of Immovable Property Decree, 1964;

(vi) The Legislative Powers Decree, 1964; na

(vii) The Cabinet Decree, 1964.

(i) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979;

(j) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984;

(k) Ripoti ya Pamoja ya Tume ya Fedha na Ripoti ya Shellukindo Juu ya Changamoto za Muungano;

(l) Ripoti ya Wangwe Juu ya Uharakishaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki;

(m) tafiti za kiuchambuzi na kitaalam zitakazofanywa na Tume; na

(n) nyaraka nyingine zozote ambazo Tume itaona ni muhimu.

(5) Tume inaweza:

(a) kwa Tanzania Bara, kumtaka Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa mamlaka ya serikali ya mitaa, Afisa Mtendaji wa Kata au Mtaa au Afisa Mtendaji wa Kijiji kuitisha mkutano wa wakazi wa mji, kata, mtaa au kijiji, kwa vyovyote itakavyo kuwa; na

(b) kwa Tanzania Zanzibar, kumtaka Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Manispaa, Katibu wa Halmashauri ya Mji au Wilaya, au Sheha kuitisha mkutano wa wakazi wa mji au Shehia mbalimbali,

kwa madhumuni ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu masuala ya Katiba kama yalivyoainishwa kwenye hadidu za rejea.

(6) Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Tume inaweza kuunda kamati na inaweza kuipatia kamati yoyote iliyoiunda kazi za jumla au kazi maalum za kufanya.

(7) Tume inaweza kumshirikisha mtu yeyote au kumtumia mtaalam mwelekezi yeyote kama itakavyokuwa lazima kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake.

(8) Isipokuwa kama mazingira yatahitaji vinginevyo, katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume itabuni utaratibu unaofanana ambao utatumika katika kila upande wa Jamhuri ya Muungano katika ukusanyaji na uchambuzi wa maoni ya wananchi, uendeshaji wa mabaraza na uandaaji wa ripoti.

(9) Yeyote atakayetaka kuendesha programu ya elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya Katiba inayotambulika na Tume atalazimika, endapo ni-

(a) mtu binafsi, kutoa taarifa kwenye Tume kwa maandishi, au kwa niaba yake, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Serikali ya Mitaa au Mkurugenzi wa Manispaa au Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya; au

(b) taasisi, jumuiya au kikundi kingine chochote cha watu wenye malengo yanayofanana, kitahitajika:

(i) kutoa taarifa kwa Tume kwa maandishi au kwa niaba yake, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Serikali ya Mitaa au Mkurugenzi wa Manispaa au Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya;

(ii) kusajiliwa chini ya sheria husika ya Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar,

na mtu huyo, taasisi, asasi, jumuiya au kikundi hicho kitalazimika pia kutoa kwa Tume, au kwa niaba yake, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Serikali za Mitaa au Mkurugenzi wa Manispaa au Katibu wa Baraza la Mji au Wilaya, kwa mtiririko huo, maelezo yanayobainisha chanzo cha fedha zitakazotumika kuendeshea programu hiyo.

(10) Taarifa inayorejewa chini ya kifungu kidogo cha (9) itaainisha muda, tarehe, mahali, eneo na aina ya mada ya programu ya elimu itakayotolewa.

(11) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, taasisi, jumuiya au makundi ya watu wenye malengo yanayofanana yanaweza kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wao kutoa maoni yao kuhusu Katiba inayopendekezwa na kisha kuyawasilisha kwenye Tume.

(12) Jumuiya yoyote, asasi, taasisi au kikundi cha watu wenye malengo yanayofanana ambacho kinataka kufanya mkutano au mkusanyiko wa hadhara kwa madhumuni ya kifungu hiki kitatoa taarifa kwenye mamlaka husika kwa kuzingatia sheria zinazosimamia uendeshaji wa mikutano au mikusanyiko hiyo.

Mabaraza ya Katiba

**18**.-(1) Kutakuwa na mabaraza ya kutoa maoni juu ya Katiba.

Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Sheria Na.2 ya mwaka 2012 kif.3

(2) Mabaraza yatatoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba na kujadili na kutoa maoni kwa kupitia mikutano itakayoitishwa na Tume.

(3) Mabaraza ya katiba yataundwa na Tume kwa muda maalum kwa kuzingatia mgawanyiko wa kijiografia wa Jamhuri ya Muungano na yatashirikisha na kuwakutanisha wawakilishi toka makundi mbalimbali ya wananchi katika jamii.

(4) Mabaraza yanayorejewa katika kifungu kidogo cha (1) na katika vifungu vingine vya Sheria hii yatakuwa maalum kwa ajili ya, na yatahudhuriwa na raia wa Tanzania pekee.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume kabla ya kukamilisha ripoti itachapisha Rasimu ya Katiba kwenye Gazeti la Serikali na magazeti mengine ili kutoa fursa kwa wananchi kusoma na kutoa maoni zaidi kwa Tume kuhusu maudhui yaliyomo kwenye Rasimu ya Katiba

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume inaweza kuruhusu asasi, taasisi au makundi ya watu kuandaa mikutano kwa ajili ya kutoa fursa kwa wanachama wake kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni hayo kwa Tume.

Ripoti ya Tume
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (o)

**19.**-(1) Kwa msingi wa mahojiano na uchambuzi uliofanywa kwa kuzingatia vifungu vya 17 na 18, Tume itatayarisha ripoti itakayokuwa na:

(a) muhtasari wa maoni ya wananachi kwa kila hadidu ya rejea;
(b) mapendekezo ya Tume kwa kila hadidu ya rejea;
(c) ripoti za wataalam waelekezi ambao Tume iliwatumia;
(d) Rasimu ya Katiba; na
(e) taarifa nyingine yoyote muhimu.

(2) Rasimu ya Katiba itakuwa ni kiambatisho kwenye ripoti ya Tume.

Uwasilishaji na uchapishaji wa ripoti

**20**.-(1) Baada ya kukamilisha kazi yake, Tume itawasilisha ripoti kwa Rais na Rais wa Zanzibar.

Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (p)

(2) Rais, ndani ya siku thelathini na moja baada ya kupokea ripoti, atachapisha Rasimu ya Katiba katika Gazeti la Serikali na kwenye magazeti mengine pamoja na maelezo kwamba Rasimu ya Katiba itawasilishwa kwenye Bunge Maalum kwa ajili ya kupitishwa Katiba inayopendekezwa.

(3) Rais baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar, atamuagiza Mwenyekiti wa Tume kuiwasilisha Rasimu ya Katiba kwenye Bunge Maalum.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3), Mwenyekiti na wajumbe wa Tume wanaweza kutoa ufafanuzi utakaohitajika wakati wa majadiliano katika Bunge Maalumu.

Makosa na adhabu Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011

Amri ya 2 aya (q) Sheria Na.2 ya mwaka 2012 kif.4

**21**.-(1) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi, atamkwamisha au kumzuia au atachochea kwa kitendo au kwa kutotenda-

(a) mjumbe wa Tume au Sekretarieti kutekeleza majukumu au mamlaka ya Tume;

(b) mtu au kundi la watu kutoa maoni kwenye Tume,

atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote-

(a) atakayefanya shughuli ya kukusanya na kuratibu maoni ya wananchi kinyume na Sheria hii;

(b) atakayejifanya kuwa mjumbe wa Tume au Sekretarieti; au

(c) atakayeendesha programu ya elimu juu ya mabadiliko ya katiba kinyume na masharti ya Sheria hii,

atakuwa ametenda kosa.

(3) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa kinyume na Sheria hii, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili.

(4) Hatua zozote zilizochukuliwa chini ya kifungu hiki hazitachukuliwa kuwa zimefikia ukomo na zitaendelea kuwa na nguvu ya kisheria hata baada ya Sheria hii kukoma kutumika.

## SEHEMU YA TANO
### KUITISHA BUNGE MAALUM

Kuitisha Bunge Maalum
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011

**22.**-(1) Kutakuwa na Bunge Maalum litakalokuwa na wajumbe wafuatao:

(a) wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;
(b) wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;
(c) wajumbe mia moja sitini na sita watakaoteuliwa kutoka:

Amri ya 2 aya (r)

(i) asasi zisizokuwa za kiserikali;
(ii) asasi za kidini;
(iii) vyama vya siasa vilivyo na usajili wa kudumu;
(iv) taasisi za elimu ya juu;
(v) makundi yenye mahitaji maalum katika jamii;

(vi) vyama vya wafanyakazi;
(vii) jumuiya ya wakulima;
(viii) jumuiya ya wafugaji; na
(ix) kikundi kingine chochote cha watu wenye malengo yanayofanana.

(2) Kwa madhumuni ya aya ya (c) ya kifungu kidogo cha (1), idadi ya wajumbe wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Zanzibar watakaopatikana kwa mujibu wa aya ya (c) haitapungua theluthi moja ya wajumbe hao.

(3) Rais, kupitia agizo katika Gazeti la Serikali atachapisha majina ya wajumbe wa Bunge Maalum.

(4) Siku ishirini na moja kufuatia kuchapishwa kwa Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa kifungu cha 20(2), Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar kwa kupitia agizo kwenye Tangazo la Serikali, litakalochapishwa kwenye Gazeti la Serikali ataitisha Bunge Maalum na kuagiza likutane tarehe itakayoainishwa kwenye Gazeti hilo.

Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum

Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (s)

**23**.-(1) Kutakuwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum watakaochaguliwa na Wajumbe wa Bunge Maalum katika kikao cha kwanza na kwa utaratibu utakaoainishwa kwenye Kanuni za Bunge Maalum.

(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum watachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Bunge Maalum kwa misingi kwamba endapo Mwenyekiti anatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano basi Makamu Mwenyekiti atakuwa mtu anayetoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti utaendeshwa kwa kura ya siri na mshindi atachaguliwa kutokana na wingi wa kura.

(4) Kabla ya kushika madaraka, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wataapa au kula yamini, vyovyote itakavyokuwa, mbele ya Katibu wa Bunge Maalum, kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria hii.

(5) Mjumbe wa Bunge Maalum hatashika madaraka yake mpaka atakapoapa au kula yamini mbele ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria hii.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, wajumbe wa Bunge Maalum watakuwa na uwezo wa kuandaa na kupitisha Kanuni za Bunge Maalum kabla ya kula kiapo au yamini, vyovyote itakayokuwa.

Katibu na watumishi wa Bunge Maalum

**24**.-(1) Mara baada ya Rais kulitangaza Bunge Maalum na kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2), Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwa mujibu wa Sheria hii, watakuwa Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum au kinyume chake.

Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (t)

(2) Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum, watashika nyadhifa zao kwa misingi kwamba, endapo Mwenyekiti atachaguliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano basi Katibu wa Bunge Maalum atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum watatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Maalum.

(4) Katibu wa Bunge Maalum baada ya kushauriana na Naibu Katibu wa Bunge Maalum watateua watumishi kutoka kwenye Bunge na Baraza la Wawakilishi kwa idadi watakayoona inafaa kwa ajili ya kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya Bunge Maalum.

(5) Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum, kabla ya kushika madaraka yao wataapa au kula yamini mbele ya Rais kwa namna ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria hii.

Mamlaka ya Bunge Maalum

**25.**-(1) Bunge Maalum litakuwa na mamlaka ya kujadili na kupitisha masharti ya katiba inayopendekezwa, kutunga masharti ya mpito na masharti yatokanayo kama Bunge Maalum litakavyoona inafaa.

(2) Mamlaka ya Bunge Maalum ya kupitisha masharti ya Katiba inayopendekezwa yatatekelezwa baada ya Rasimu ya Katiba kuwasilishwa na Mwenyekiti wa Tume na kupitishwa na Bunge Maalum.

Masharti kuhusu Bunge Maalum

**26**.-(1) Bunge Maalum litatunga kanuni kwa ajili ya kuendesha shughuli za Bunge Maalum.

(2) Ili Katiba inayopendekezwa iweze kupitishwa katika Bunge Maalum, itahitaji kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya idadi ya wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya idadi ya wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Zanzibar.

Sheria za Bunge Maalum Sura ya 1

**27**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria yoyote ya Bunge Maalum, Sheria ya Tafsiri za Sheria itatumika katika kutoa tafsiri kwa Sheria ya Bunge Maalum na kwamba rejea kwenye Sheria hiyo au sheria nyingine yoyote, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo, itajumuisha rejea kwenye Sheria ya Bunge Maalum.

Sura ya 2 na Sura ya 296

(2) Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge Maalum, kama itakavyoelezwa kwenye Kanuni za Bunge Maalum.

Ukomo wa mamlaka ya Bunge Maalum
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (u)

**28**.-(1) Baada ya kutunga Katiba inayopendekezwa, masharti yatokanayo na masharti ya mpito, Bunge Maalum litavunjwa na mamlaka ya kutunga masharti ya Katiba inayopendekezwa, masharti yatokanayo na masharti ya mpito yatakoma.

(2) Kuvunjwa na kukoma kwa mamlaka ya Bunge Maalum hakutachukuliwa kuwa kunaondoa mamlaka ya Rais kuliitisha tena Bunge hilo kwa lengo la kuboresha masharti yaliyomo kwenye Katiba inayopendekezwa.

Gharama za Bunge Maalum
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (v)

**29**.-(1) Gharama za Bunge Maalum kwa mujibu wa Sheria hii, zitalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Wajumbe wa Bunge Maalum, Katibu na Watendaji watalipwa kwa namna ambayo Rais, kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zilizopo, ataamua.

Ukaguzi wa Hesabu za Bunge Maalum
Tangazo la Serikali Na. 394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (w)

**30.**-(1) Katibu wa Bunge Maalum atahakikisha kwamba vitabu vya hesabu vinahifadhiwa na atahakikisha kwamba, ndani ya muda usiozidi miezi mitatu baada ya kwisha mwaka wa fedha wa Serikali, taarifa ya mapato na matumizi katika mwaka wa fedha husika inaandaliwa.

Sura ya 418, 410 na 348

(2) Hesabu zinazohusu kazi za Tume hadi siku ya mwisho ya mwaka wa fedha wa Serikali zitawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sheria ya Ununuzi wa Umma na Sheria ya Fedha za Umma.

## SEHEMU YA SITA
### UHALALISHAJI WA KATIBA INAYOPENDEKEZWA

Uendeshaji wa kura ya maoni Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (x)

**31**.-(1) Kwa madhumuni ya kuyapatia uhalali masharti yaliyomo kwenye Katiba inayopendekezwa, kutakuwa na kura ya maoni itakayoandaliwa, kuendeshwa na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

(2) Katika utekelezaji wa kifungu kidogo cha (1), Tume ya Uchaguzi Zanzibar itaandaa, kuendesha na kusimamia upigaji wa kura ya maoni, kisha itawasilisha kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi matokeo ya kura zilizopigwa Tanzania Zanzibar kwa ajili ya kutangazwa.

Swali la kura ya maoni Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (y)

**32**.-(1) Ndani ya siku saba baada ya kuchapishwa Katiba inayopendekezwa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar itatayarisha na kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali swali litakaloamuliwa kwa kura ya maoni.

(2) Swali linalorejewa katika kifungu kidogo cha (1), litatayarishwa baada ya mashauriano na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano akishirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

(3) Swali litakaloulizwa katika kura ya maoni litamtaka mpiga kura kuonyesha kuwa anaridhia au kutoridhia Katiba inayopendekezwa na litatayarishwa kwa namna ambayo litamtaka mpiga kura kujibu “Ndiyo” au “Hapana”.

(4) Upigaji kura ya maoni utakuwa wa siri.

Taarifa ya uendeshaji wa kura ya maoni
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (z)

**33**.-(1) Ndani ya siku kumi na nne baada ya kuchapishwa kwa swali katika Gazeti la Serikali, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar itatangaza taarifa inayoainisha**:**

(a) siku ambayo kura ya maoni itafanyika;

(b) muda wa upigaji kura ya maoni; na

(c) muda wa kuelimisha na kuhamasisha wananchi kupiga kura ya maoni juu ya Katiba inayopendekezwa.

(2) Kwa madhumuni ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu kuipigia kura ya maoni Katiba inayopendekezwa, Tume italazimika, na vyama vya siasa na vyama vya kijamii vinaweza kutoa elimu ya uraia na uhamasishaji juu ya Katiba inayopendekezwa kwa muda usiozidi siku thelathini kuanzia siku ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(3) Ndani ya siku ishirini na moja baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutangaza taarifa, msimamizi wa uchaguzi wa kila jimbo la uchaguzi atawataaarifu wananchi wa eneo analohusika nalo kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa kura za maoni.

Haki ya kupiga kura katika kura ya maoni
Sura ya 343 Sheria Na.11 ya 1984(Z)
Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (aa)

**34**. Mtu yeyote ambaye jina lake limeingizwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililoanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 1984, atakuwa na haki ya kupiga kura, isipokuwa kama mtu huyo atakuwa amezuiwa kupiga kura na sheria nyingine yoyote.

Utaratibu wa kuendesha kura ya maoni Sura ya 343, 292 Sheria Na.11 ya 1984(Z)

**35**. Utaratibu wa uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kwa kufanya marekebisho yatakayolazimu, utatumika katika kuendesha kura ya maoni kwa mujibu wa Sheria hii.

Matokeo ya kura ya maoni Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011

Amri ya 2 aya (bb)

**36**.-(1) Matokeo ya kura ya maoni yataamuliwa kutokana na wingi wa kura zote halali zitakazopigwa kwa swali litakalopigiwa kura ya maoni na matokeo yatakayotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi yataheshimiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Matokeo ya kura ya maoni yataamuliwa kwa msingi wa kuungwa mkono kwa asilimia inayozidi hamsini ya jumla ya kura zote zilizopigwa kutoka Tanzania Bara na asilimia inayozidi hamsini ya jumla ya kura zote zilizopigwa kutoka Tanzania Zanzibar.

(3) Endapo kura za "NDIYO" juu ya swali la kura ya maoni hazitazidi asilimia hamsini ya kura zote halali zilizopigwa kwa Tanzania Zanzibar au Tanzania Bara au zote pamoja, Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa kukubaliana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti la Serikali, itateua siku nyingine ndani ya siku thelathini baada ya kutangazwa matokeo ya kura ya maoni, ya kurudiwa kwa upigaji kura ya maoni na taratibu za kupiga kura zitaanza upya.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kukubaliana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, pale ambapo mazingira yatahitaji:

(a) kutoa muda unaotosha kwa ajili ya uhamasishaji wa wananchi juu ya upigaji kura ya maoni ya Katiba inayopendekezwa; au

(b) kutoa muda utakaoonekana unafaa kwa Rais kwa kukubaliana na Rais wa Zanzibar kuitisha upya Bunge Maalum kwa madhumuni ya kuboresha masharti ya Katiba inayopendekezwa.

(5) Endapo wingi wa kura ya maoni utakuwa ni "HAPANA", Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, itaendelea kutumika.

Kuvunjwa kwa Tume Tangazo la Serikali Na.394 la mwaka 2011 Amri ya 2 aya (cc)

**37**.-(1) Baada ya matokeo ya kura ya maoni kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Rais kwa kupitia amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, ataivunja Tume.

(2) Kuvunjwa kwa Tume kwa amri ya Rais kutakuwa na maana ya ukomo wa mamlaka ya Tume na Sekretarieti.

Kuanza kutumika kwa Katiba

**38**.-(1) Masharti ya Katiba Mpya yataanza kutumika tarehe itakayotajwa kwenye Katiba hiyo.

(2) Rais atazindua, kwa namna atakayoona inafaa, kuanza kutumika kwa Katiba Mpya.

(3) Baada ya kuzinduliwa kwa Katiba Mpya, Sheria hii itakuwa imemaliza matumizi yake na itapoteza nguvu ya kisheria.

(4) Katika matumizi ya Sheria hii, toleo la lugha ya Kiswahili na toleo la lugha ya Kiingereza yote ni sahihi.

______

JEDWALI LA KWANZA

______

*(Chini ya kifungu cha (11)*

______

SEHEMU YA I
KIAPO/YAMINI YA MJUMBE WA TUME

Mimi ……………………………………………………………………………….. nikiwa nimeteuliwa na Rais kuwa …………………………………tarehe ………………………… siku ya ……………………………………………….. 2011 kufanya kazi za Mjumbe wa Tume, naapa/nathibitisha kwamba nitakuwa mtiifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bila upendeleo na kwa kadri ya uwezo na ufahamu wangu, nitatimiza wajibu wangu na kufanya kazi zinazonihusu kama Mjumbe wa Tume.

Ewe Mungu nisaidie.

………………….
Mjumbe wa Tume

SEHEMU YA II
KIAPO/YAMINI YA KATIBU/NAIBU KATIBU

Mimi …………………………………….. nikiwa nimeteuliwa na Rais kuwa …………………………… tarehe ……………………….. siku ya ………………..20…. kufanya kazi za Katibu/Naibu Katibu, naapa/nathibitisha kwamba nitakuwa mtiifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bila upendeleo na kwa kadri ya uwezo na ufahamu wangu, nitatimiza wajibu wangu wa kufanya kazi zinazonihusu kama Katibu/Naibu Katibu.

Ewe Mungu nisaidie.

………………………
KATIBU

JEDWALI LA PILI

(*Chini ya kifungu cha 12(2))*

KANUNI ZA MAADILI YA WAJUMBE WA TUME NA SEKRETARIETI

1. Kila mjumbe wa Tume/Sekretarieti atapaswa kufanya kazi zake kwa uadilifu bila ya upendeleo na bila kuingiliwa na atafanya kazi za ofisi yake kwa nia njema na bila woga, upendeleo au chuki.

2. Mjumbe wa Tume/Sekretarieti katika kipindi cha kutumikia nafasi yake, hatakuwa na sifa ya kuteuliwa au kuchaguliwa kwenye nafasi yoyote ya kisiasa.

3. Mjumbe wa Tume/Sekretarieti-
   (a) kupitia ujumbe wake, hatoshiriki, hatatoa kauli, kufanya matendo au kwa namna yoyote ile kuhatarisha uhuru wa mjumbe au kuathiri hadhi, uadilifu, uhuru au hadhi ya Tume/Sekretarieti; au
   (b) kutumia kwa manufaa yake au kufaidika na taarifa yoyote ya siri akiwa kama mjumbe wa Tume/Sekretarieti.

JEDWALI LA TATU

(*Chini ya kifungu cha 24(5)*

KIAPO/YAMINI YA KATIBU/NAIBU KATIBU WA BUNGE MAALUM

Mimi …………………………………………………………………… nikiwa nimeteuliwa siku ya ………………..20…. kwa mujibu wa Sheria kufanya kazi za Katibu/Naibu Katibu wa Bunge Maalum, naapa/nathibitisha kwamba nitakuwa mtiifu na bila upendeleo na kwa kadri ya uwezo na ufahamu wangu, nitatimiza wajibu wangu wa kufanya kazi zinazonihusu kama Katibu/Naibu Katibu wa Bunge Maalum.

Ewe Mungu nisaidie.

……………………

KATIBU WA BUNGE MAALUM

JEDWALI LA NNE

(*Chini ya kifungu cha 23 (4)(5)*

KIAPO CHA MWENYEKITI/MAKAMU MWENYEKITI NA WAJUMBE WA BUNGE MAALUM

Mimi ……………………………………….……………….. nikiwa nimeteuliwa kuwa Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti/Mjumbe wa Bunge Maalum, naapa/nathibitisha kwamba nitakuwa mwaminifu na mtiifu kwa Jamhuri ya Muungano na kwa kadri ya uwezo na ufahamu wangu, nitatimiza wajibu wangu na kufanya kazi zinazonihusu bila ya upendeleo, na bila ya kukiuka Sheria za nchi.

Ewe Mungu nisaidie

______________________________

Mwenyekiti/Makamu Mwenyekiti/Mjumbe wa Bunge Maalum